JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**KATIKA KAMATI YA MALALAMIKO**

LALAMIKO NA: TCRA/LAL/01/12/OKTOBA/2018

KATI YA

**MARCO MISANA..........................................................................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

**MIC (T) LIMITED....................................................................MLALAMIKIWA**

MBELE YA:

| | | |
|---|---|---|
| Valerie N Msoka | - | Mwenyekiti |
| Dr. Mzee Mndewa | - | Mjumbe |
| Jehovannes Zacharia | - | Mjumbe |

# UAMUZI

29 NOVEMBA, 2018

**UAMUZI WA SHAURI KATI YA MARCO MISANA DHIDI YA MIC (T) LIMITED**

Bwana MARCO MISANA ambaye anatambuliwa kama Mlalamikaji katika shauri hili ni mteja wa Mlalamikiwa MIC (T) LIMITED (Tigo). Mlalamikiwa amepewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutoa huduma ya mawasiliano.

Mlalamikaji alileta malalamiko katika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania akidai shillingi za Tanzania milioni mia moja na hamsini tu (TZS 150,000,000/=), ikiwa ni fidia kwa kukosa mawasiliano kutokana na Mlalamikiwa kusitisha huduma hiyo katika namba 0713 354 572 ambayo Mlalamikaji anadai kuimiliki.

Shauri hili lilipokuja mbele ya Kamati ya Malalamiko kwa usikilizwaji tarehe 12 Oktoba, 2018 Mlalamikaji alifika akiambatana na wakili wake Bwana Lulinga Jonathan Lulinga wa Jonvil Advocates, ambapo walikuwa na mashahidi wawili ambao ni Maria M. Humuli kutoka kampuni ya Bluered Security Limited na Dotto Mfaume kutoka kampuni ya Anaconda Security Services Limited. Upande wa Mlalamikiwa uliwakilishwa na Bwana Tumaini Shija ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa kampuni ya MIC Tanzania Ltd.

Mlalamikaji akiwa kama shahidi wa kwanza, akiongozwa na wakili Lulinga Jonathan Lulinga aliieleza Kamati hii kuwa yeye ni Mkurugenzi wa kampuni ya ulinzi kwa jina la Anaconda Security Services Limited, majukumu ya kazi yake ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wateja hususan wale wa shughuli za ulinzi.

Alieleza kuwa awali alikuwa akifanya kazi katika kampuni ya Bluered Security Limited na alitoa mkataba wa ajira kama ushahidi. Aliiambia Kamati kuwa majukumu yake ya kikazi alipokuwa Bluered Security yalikuwa ni kuwasiliana na wateja pamoja na walinzi. Akiwa katika nafasi hiyo namba yake ya simu aliyokuwa akitumia 0713 354 572 iliunganishwa na huduma ya kulipia baada ya kupata huduma (post-paid) na mwajiri wake ndiye alikuwa analipia huduma hiyo.

Mnamo tarehe 9/5/2018 aliandika barua ya kuacha kazi na kukubaliwa, kimaandishi, bila pingamizi. Mlalamikaji alitoa barua zote mbili kama ushahidi wake. Kuanzia tarehe

01/06/2018 alianza kazi rasmi katika kampuni yake mpya ya Anaconda Security Services Limited.

Mnamo tarehe 6/6/ 2018 akiwa katika kazi zake, ghafla mawasiliano yalikata katika namba yake aliyokuwa akitumia ambayo ni 0713-354572 na alipojaribu kutumia simu nyingine kupiga namba hiyo alijulishwa kuwa simu haipatikani. Mlalamikaji anadai kuwa alikaa usiku mzima bila Mawasiliano na ilipofika asubuhi siku iliyofuata alikwenda katika ofisi za Bluered ili kubaini tatizo. Alijulishwa kuwa Bluered waliiandikia Tigo barua kusitisha huduma ya kulipia baada ya huduma (post-paid) katika namba ya Mlalamikaji baada ya kuwa ameacha kazi. Tarehe 7/6/2018 Mlalamikaji alidai kuwa alitakiwa aende Singida kikazi lakini alishindwa kwa kutokuwa na mawasiliano.

Mlalamikaji anadai kuwa namba yake hiyo alikuwa akiitumia siku nyingi toka kipindi cha Mobitel-Buzz mpaka leo Tigo. Namba hiyo imesajiliwa lakini alishangaa Tigo kuifungia namba hiyo bila kumpa taarifa yeyote. Madhara aliyoyapata kutokana na kutokuwa na mawasiliano ni pamoja na kupoteza wateja Singida na Mbeya ambapo amepoteza zaidi ya million 150 pesa za Tanzania.

Mlalamikaji aliendelea kueleza kuwa aliwaandikia Tigo barua ya madai kupitia mwanasheria wake, na Tigo pia walimjibu barua hiyo. Barua zote mbili zilitolewa kama ushahidi wa upande wa Mlalamikaji. Alimaliza kwa kuomba Kamati imwamuru Mlalamikiwa kumlipa fidia maalum ya Tshs 150 000 000/=, gharama za mwanasheria pamoja na fidia za ujumla Tshs 200, 000, 000.

Katika mahojiano na mwakilishi wa Mlalamikiwa, Mlalamikaji alieleza kuwa kwa sasa ana namba nyingine ya Airtel baada ya namba ile ya Tigo kufungiwa. Mlalamikaji alieleza kuwa, anafahamu kuwa mwaka 2010 ilipitishwa Sheria ya kutaka namba zote za simu zisajiliwe. Alisisitiza kuwa alikuwa akimiliki namba yake mwenyewe na sio kampuni ya Bluered Security. Alidai kuwa baada ya kubaini namba yake imefungwa alienda ofisi za Bluered kwa sababu alikuwa mwajiriwa wake na alikuwa akitumia namba hiyo akiwa ofisini kwao. Hata hivyo alisema kuwa hakuwa na kielelezo chochote cha kuonesha kuwa alipoteza wateja na pato na kwamba hakuweza kutafuta line nyingine kwani alikuwa na shughuli ya kufuatilia namba yake iliyokuwa imefungwa.

Alipohojiwa na Kamati alieleza kuwa alikuwa anategemea kupata kazi ambayo ingempatia kipato cha Tshs 150,000,000. Alisajili namba hiyo ya Tigo kabla ya mwaka 2015 kwa kutumia kitambulisho cha uraia, hata hivyo hakumbuki kitambulisho cha uraia alikipata lini. Aliongeza kuwa namba ya mteja wa Singida alikuwa nayo lakini aliamua kufuatilia laini badala ya safari.

Shahidi wa pili wa Mlalamikaji Bi Maria Humuli, Afisa rasilimali watu wa Bluered Security Limited, akiongozwa na Wakili wa Mlalamikaji, Bwana Lulinga Jonathan Lulinga, alieleza kuwa anamfahamu Mlalamikaji kwa kuwa alikuwa ni mfanyakazi mwenzake katika kampuni ya Bluered Security Limited ambapo amefanya kazi kwa muda wa miaka mitatu, na ya kwamba Mlalamikaji alikuwa akipata huduma ya mawasiliano na usafiri kwa gharama za kampuni. Shahidi alieleza kuwa, katika huduma ya Mawasiliano, Mlalamikaji aliunganishwa katika huduma ya malipo ya baada ya matumizi (post-paid) ya kampuni ya mawasiliano ya Tigo chini ya mkataba kati ya Tigo na Bluered Security Limited. Alidai kuwa namba binafsi ya mwajiriwa ndiyo iliunganishwa na huduma hiyo. Hata hivyo aliieleza Kamati kuwa kwa sasa Mlalamikaji si mwajiriwa wa Bluered Security Limited, kwani Mlalamikaji aliacha kazi kwa hiari yake.

Shahidi Bi Maria Humuli, aliendelea kueleza kuwa, baada ya Mlalamikaji kuacha kazi katika kampuni ya ulinzi ya Bluered Security Limited, kampuni hii iliwaandikia barua MIC (T) Limited ikitakiwa kusitisha huduma ya malipo ya baada katika namba inayolalamikiwa. Ijapokuwa shahidi huyu hakuleta barua hiyo katika Kamati hii, aliweza kuitambua barua iliyotolewa na Mlalamikiwa kuwa ndiyo hiyo iliyoandikwa na kampuni yake.

Katika mahojiano baina yake na mwakilishi wa Malamikiwa, shahidi huyu alieleza kuwa Mlalamikaji alikuwa ni mfanyakazi mwenzake ambaye mara ya mwisho kuonana naye ni pale alipokuja kuleta malalamiko ofisini kwao kuhusu kufungiwa kwa laini yake. Alieleza kuwa yeye ndiye aliyepeleka barua Tigo baada ya kutumwa na bosi wake bwana Silayo na alirudi mara ya pili kuulizia. Shahidi huyu pia alitambua barua iliyopelekwa Tigo kutoka Bluered Security Limited na kudai kuwa hapingani na kilichomo kwenye barua

hata hivyo hakuja na barua iliyoandikwa na Bluered Security kuomba kuunganisha namba ya Mlalamikaji katika huduma ya post-paid.

Shahidi wa tatu wa Mlalamikaji Bwana Dotto Ally Mfaume, mtaalamu wa masuala ya TEHAMA, meneja wa operesheni (IT and Operational Manager) wa kampuni ya Anaconda Security Services Limited, akiongozwa na wakili Lulinga Jonathan Lulinga shahidi alieleza kuwa amfahamu Mlalamikaji kwani ni bosi wake katika kampuni ya Anaconda Security Services Limited. Shaidi alieleza hasara ambazo ofisi imepata kutokana na Mlalamikaji kutokuwa na mawasiliano ni kupoteza kazi na wateja.

Katika mahojiano na mwakilishi wa Mlalamikiwa, shahidi huyu alieleza kuwa ofisi yao kwa sasa wana simu ya mkononi, ambapo hata yeye pia anasimu ya mkononi. Shahidi aliieleza Kamati kuwa alianza kazi katika kampuni ya Anaconda Security Services Limited kati ya tarehe 6 - 7 mwezi wa sita mwaka huu. Shahidi pia aliieleza Kamati kuwa yeye alimshauri Mlalamikaji aende ofisi za Tigo baada ya tukio lakini hajui kama Mlalamikaji alifanya kama alivyomshauri au la. Hata hivyo, alipohojiwa juu ya kuwa na uthibitisho wa upotevu wa wateja alijibu kuwa hakuwa na uthibitisho wowote. Alidai pia kuwa Mlalamikaji anawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu, Bwana Misango, ambaye ndiye anahusika na mambo ya fedha. Aliiambia Kamati hii kuwa ni wateja wa kampuni ndiyo waliopotea na sio wateja wa Mlalamikaji, na hata hasara pia inayodaiwa katika shauri hili ni hasara ambayo kampuni ya Anaconda Security Services Limited imeipata kutokana na Mlalamikaji kukosa mawasiliano.

Katika mawasilisho ya mwisho yaliyofanywa na wakili wa Mlalamikaji, Bwana Lulinga Jonathan Lulinga, aliwasilisha kuwa Tigo imefanya uzembe kwenye kukata mawasiliano ya mteja wake ambaye mpaka sasa hana mawasiliano. Na kuomba maombi ya mteja wake yasikilizwe.

Kwa upande wa Mlalamikiwa akiwakilishwa na Bwana Tumaini Shija Afisa Sheria Mkuu wa kampuni ya MIC Tanzania Limited (Tigo), alieleza kuwa baada ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielectroniki na Posta kuanza kutumika mwaka 2010, usajili wa namba za simu umekuwa ni lazima. Namba 0713 354572 ni namba ambayo Mamlaka ya

Mawasiliano Tanzania imempa Tigo, na kwamba namba hiyo inatakiwa kusajiliwa kisheria. Mfumo wa huduma ya malipo ya baada (post-paid) hutolewa na Tigo kwa wateja ambao ni wa kampuni. Mteja hujaza fomu za maombi kwa namba anazotaka kusajili kwa huduma hiyo na hutakiwa kuweka dhamana ya pesa.

Bwana Shija alieleza kuwa namba 0713 354572 inamilikiwa na Bluered Security Limited chini ya utambulisho wa huduma ya malipo ya baada (post-paid). Aliwasilisha nakala ya mkataba baina ya Tigo na Bluered Security Limited ikiambatana na nakala ya fomu ya maombi, nakala ya Leseni ya biashara ya Bluered Security Limited pamoja na nakala ya kitambulisho cha Mkurugenzi wa Bluered Security Limited, ambazo zilitumika kufanya usajili wa namba kadhaa ikiwemo namba inayolalamikiwa. Alieleza kuwa barua ya bwana Silayo ambaye ni Mkurugenzi wa Bluered Scerurity Limited ilielekeza kuwa namba 0713 354572 iondolewe katika huduma ya malipo ya baada (post-paid) na pia isitishwe. Mwakilishi wa Mlalamikiwa aliiambia Kamati kuwa Mlalamikiwa haimtambui Mlalamikaji kama mmiliki wa namba inayolalamikiwa, na kwamba Mlalamikaji aliposhauriwa asajili namba hiyo alikataa na kudai mpaka kesi imalizike.

Katika mahojiano na wakili wa Mlalamikaji, Mwakilishi wa Mlalamikiwa alieleza kuwa yeye ni mwanasheria wa kampuni ya Tigo na kuwa anazifahamu sheria zinazoongoza kampuni ikiwemo Sheria ya Mawasiliano ya Kielectroniki na Posta ya mwaka 2010. Alieleza kuwa haiwezekani mtu kutumia simu bila kusajili, na kwamba usajili wa kampuni unahitaji vitu mbalimbali ikiwemo mkataba wa kujiunga na malipo ya baada ya kupatiwa huduma. (post-paid). Hakuwa na ushahidi wowote kwamba namba zilizounganishwa kwa huduma ya malipo ya baada (post-paid) kwa kampuni ya Bluered zilikuwa hazijasajiliwa. Aliendelea kueleza kuwa fomu aliyoitoa mbele ya Kamati ni ya usajili wa huduma ya malipo ya baada (post-paid) na si usajili wa laini ya simu, na kuwa barua iliyowasilishwa inahusu kuondelewa katika huduma kwa namba inayolalamikiwa. Bwana Shija aliendelea kueleza kuwa kwa sasa taarifa zilizopo kwenye mtandao wa Tigo kuhusu namba 0713 354572 ni kwamba namba hiyo haipo. Hata hivyo alikiri kuwa yeye kama mwanasheria wa Mlalamikiwa hahusiki na usitishaji huduma ya mawasiliano kwa Mlalamikaji wala kwa wengine wowote, kwani siyo sehemu ya kazi yake.

Katika mawasilisho ya mwisho mwanasheria wa Mlalamikiwa alieleza kuwa Mlalamikaji ameshindwa kuithibitishia Kamati kuwa anao usajili wa namba inayolalamikiwa na kuwa yeye ni mmiliki halali wa namba hiyo. Pili MIC Tanzania Limited (Tigo), haikuzembea kwenye jambo hili, isipokuwa ilitekeleza maelekezo ya mteja wake aliyekuwa anatumia namba inayolalamikiwa, ambaye ni Bluered Secuirty Limited. Tatu, ni kuwa Mlalamikaji hakuwahi hata siku moja kufuatilia suala hilo kwa Mlalamikiwa kwa sababu alijua kuwa namba hiyo ni ya Bluered Security Limited.

Kuhusu madhara na hasara alizopata Mlalamikaji, Mwanasheira wa Tigoi alieleza kuwa ameshindwa kuthibitisha mbele ya Kamati hasara alizopata yeye binafsi, uhusiano wa namba binasfi na hasara iliyopata kampuni ya Anaconda Security Services Limited, na kwa nini hakutumia simu ya kampuni kuwasiliana na wateja wa kampuni. Mlalamikiwa aliieleza Kamati kuwa, Mlalamikaji hakuweza kuleta mbele ya Kamati ushahidi wa hasara yoyote inayohusiana na lalamiko lake. Alihitimisha kwa kuomba Kamati kutupilia mbali malalamiko ya Mlalamikaji kwani hayana uhalali.

Kamati hii baada ya kusikiliza ushahidi wa Mlalamikaji pamoja na utetezi wa Mlalamikiwa ilibaini kuwa ni jambo lisilokuwa na ubishi kuwa Mlalamikiwa MIC (T) Limited alisitisha huduma ya mawasiliano katika namba 0713 354572. Baada ya hapo Kamati hii ilijielekeza katika hoja zifuatazo,

1. Nani alikuwa mmiliki halali wa namba 0713 354572 wakati Mlalamikiwa anasitisha huduma ya mawasiliano katika namba hiyo.
2. Kama usitishwaji wa huduma ya mawasiliano katika namba 0713 354572 ulifanyika kwa kufuata taratibu.
3. Kama Mlalamikaji anastahili kulipwa fidia kama alivyodai.

Katika kuangalia ni nani alikuwa mmiliki halali wa namba inayolalamikiwa wakati Mlalamikiwa anasitisha huduma ya mawasiliano, Mlalamikaji alidai katika ushahidi wake kuwa alikuwa akimiliki namba hiyo hata kabla ya kuanza kazi katika kampuni ya ulinzi ya Bluered Secuirty Limited na kwamba baada ya kuajiriwa na Bluered namba hiyo iliunganishwa katika huduma ya malipo ya baada (post-paid) iliyokuwa inatolewa na Mlalamikiwa kwa kupitia mkataba baina yake na kampuni ya Bluered Secuirty Limited.

Mlalamikaji alidai kuwa alisajili namba hiyo kwa jina lake hata hivyo hakutoa kielelezo chochote kuthibitisha usajili wake. Upande wa Mlalamikiwa ulidai kuwa namba hiyo ilikuwa inamilikiwa na kampuni ya ulinzi ya Bluered Secuirty Limited na alitoa mkataba baina ya Mlalamikiwa (MIC (T) Limited) na Bluered Security Limited, ambapo kupitia mkataba huo namba 0713 354572 iliunganishwa katika huduma ya post-paid.

Kamati hii imejiridhisha kuwa Mlalamikaji baada ya kuajiriwa, alisalimisha namba 0713 354572 kwa hiari yake kwa mwajiri wake ambaye ni Bluered Securtiy Limited, ambaye aliingiza kwenye mkataba wa kampuni ya MIC Tanzania Limited na kuwa walikuwa wanaihudumia kwa mujibu wa mkataba hadi walipo omba kusitishiwa huduma kwenye namba husika.

Kamati ilibaini kuwa mwajiri huyo asingeweza kuingza katika mkataba unaohusu namba ya simu inayodhaniwa kuwa ni ya Mlalamikaji bila ya ridhaa yake, na iwapo ilikuwa hivyo, basi Mlalamikaji angelalamika tangu ilipoingizwa kwenye mkataba na mwajiri wake wa zamani.

Hivyo Kamati hii imebaini kuwa, kampuni ya Bluered Securtiy Limited ndio iliyokuwa na udhibiti (control) ya laini hiyo kutokana na mkataba na Tigo. Aidha, umiliki wa laini uliendelea kuwa kwa Mlalamikaji.

Katika hoja ya pili, juu ya kufuatwa kwa taratibu katika kusitisha huduma ya mawasiliano katika namba 0713 354572. Kamati hii imebaini kuwa barua Iliyoandikwa na Bluered Securtiy Limited kwa Tigo ilikuwa bayana ikiitaka Tigo kuondoa laini ya Mlalamikaji kwenye orodha ya laini za simu ambazo Bluered Securtiy Limited iliingia Mkataba wa malipo ya baada na Tigo. Aidha, ilibainika kuwa, Tigo haikufanya kile tu kilichoelekezwa kwenye barua bali iliikatia laini hiyo Mawasiliano.

Kuhusu hoja ya uhalali wa Mlalamikaji kulipwa fidia, Kamati hii imezingatia maelezo ya wa shahidi wa Mlalamikaji Bwana Dotto Ally Mfaume ambako kuhusiana na hasara ambayo Mlalamikaji anadai alipata na kudai fidia ni hasara ambayo Kampuni ya Anakonda Security Services Limited ilipata.

Kamati pia, imetilia maanani ukweli kuwa, baada ya Mlalamikaji kutambua laini kufungiwa na kutakiwa kufika katika ofisi ya Tigo, jambo ambalo hata Mlalamikaji mwenyewe alikiri, alifika lakini alikataa maagizo aliyopewa ya kusajili upya laini yake.

Kamati imezingatia kuwa kampuni ni mtu tofauti kisheria ambaye anauwezo wa kudai na kudaiwa. Hivyo basi, hata kama Mlalamikaji angethibitisha kuwa alikuwa ni mmiliki halali wa namba 0713 354572 na pia namba hiyo ilisitishwa mawasiliano na Mlalamikiwa kinyume na taratibu, bado Mlalamikaji katika shauri hili hana mamlaka ya kudai fidia kwa niaba ya kampuni ya ulinzi ya Anaconda Security Services Limited.

Kufuatana na maelezo hayo hapo Kamati imeona kuwa, malalamiko ya Mlalamikaji katika shauri hili hayana mashiko na kuyatupilia mbali.

Mlalamikaji na Mlalamikiwa kila mmoja atawajibika kwa gharama zake mwenyewe.

Mlalamikiwa na Mlalamikaji wote wana haki ya kukata rufaa katika Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal – FCT) ndani ya siku 21 baada ya kupokea uamuzi huu endapo hawataridhishwa na Uamuzi ya Kamati hii.

Imetolewa leo tarehe **29** mwezi **Novemba, 2018 Dar es Salaam**

..................................................................

Valerie N. Msoka
**MWENYEKITI**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA